## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KUJADILI TAARIFA ZA MWEZI NOVEMBA 2021 KILICHOFANYIKA TAREHE 23.12.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI.

### A: WAHESHIMIWA MADIWANI WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yanga E. Makaga | M/kiti – H/W | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Makoye L. Sengerema | M/Kiti Kamati ya Kudhibiti UKIMWI | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Fortunatus Nzwagi | M/Kiti Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira | " |
| 4. | Mhe. Enock S. Ndekeja | M/Kiti Kamati ya Maadili | " |
| 5. | Mhe. Mathias H. Mashauri | M/Kiti Kamati ya Elimu, Afya na Maji | " |
| 6. | Mhe. Betty Dacman | Diwani Viti Maalum | " |
| 7. | Mhe. Modesta L. Bulugu | Diwani Viti Maalum | " |
| 8. | Mhe. Mbugai Majumba | Diwani Kata ya Mission | " |
| 9. | Mhe. Tryphone S. Male | Diwani Kata ya Kasenyi | " |
| 10. | Mhe. Tabasam H. Mwagao | Mbunge | " |

### B: WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

Hakuna

### C: WATAALAM WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Binuru M. Shekidele | Mkurugenzi Mtendaji(W) | Katibu |
| 2. | Ndg. Alan Augustine | Katibu Tawala (W) | |
| 3. | Ndg. Ndaro Samson | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | |
| 4. | Ndg. Anociatha B. Missingo | Kny. Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali watu | |
| 5. | Ndg. Prosper Luasha | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | |
| 6. | Ndg. Deocles Mushema | Kny. Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha | |
| 7. | Ndg. Ashura Kajuna | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi | |
| 8. | Ndg. Serapian Matiku | Kaimu Mkuu Kitengo cha Sheria | |
| 9. | Ndg. Mwita M. Waryuba | Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | |
| 10. | Dr. Saumu Kumbisaga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya | |
| 11. | Ndg. Dickson N. Nyamwitagi | Kny Mkuu wa Idara ya Usafishaji na Mazingira | |
| 12. | Ndg. Boniphace Kasasiro | Kny Kaimu Mkuu Idara ya Maendeleo ya Jamii | |

| | | |
|---|---|---|
| 13. | Ndg. Edgar Heri | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 14. | Ndg. Donati M. Bunonosi | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 15. | Ndg. Neema M. Ndekirwa | Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 16. | Ndg. Fadhila W. Abel | Afisa Tarafa ya Sengerema |
| 17. | Ndg. Charles P. Ntamuti | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 18. | Benadetha S. Fransisco | Mkuu Kitengo cha Ufugaji Nyuki |
| 19. | Ndg. John Mwita | Kaimu Mkuu Kitengo cha Ugavi na Manunuzi |
| 20. | Ndg. Peter C. Mkalipa | Kaimu Mkuu Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 21. | Ndg. Joshua Jacob | Kny Afisa Usafirishaji |
| 22. | Ndg. Paschal W. Mafuru | Mhandisi |

**D: WAANDISHI WA VIKAO**

1. Ndg. Fidelis S. Elias
2. Ndg. Magreth M. Paul
3. Evance M. Paul

**Muht.Na.64/12/2021- Kufungua Kikao**

**Katibu:** Aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwaeleza kwamba kikao hicho ni kwa ajili ya kujadili taarifa za mwezi Novemba 2021. Aliwatambulisha watumishi walioripoti kuanza kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema akiwemo Mhandisi Paschal Mafuru na Mhasibu Deocles Mushema kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufungua kikao.

**Mwenyekiti:** Alianza kwa kusoma Sala ya Halmashauri na kisha aliwakaribisha wajumbe kwenye kujadili agenda za kikao. Naye pia aliwakaribisha Mhandisi na Wahasibu walioripoti kufanya kazi Katika Halmashauri ya Sengerema. Aliweka bayana kuwa hafurahii kuona baadhi ya wataalam wakihangaika rumande kwa kosa ambalo si lao. Alimshauri Mkurugenzi aangalie namna ya kufanikisha dhamana kwa wataalam hao kisha alikifungua kikao mnamo saa 8:10 mchana.

**Muht.Na.65/12/2021- Kuthibitisha Agenda za Kikao**

Wajumbe wote kwa pamoja walithibitisha agenda za kikao zifuatazo:

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda za Kikao
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 17.11.2021
4. Yatokanayo na Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 17.11.2021
5. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Dharula cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 22.10.2021
6. Taarifa ya Mapato na Matumizi Mwezi Novemba 2021
7. Taarifa ya Motor Grader 140K SM11110 ya Halmashauri kwa Kipindi cha Mwezi Novemba 2021
8. Taarifa ya mapokezi ya fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha Tsh 886,012,138.30
9. Taarifa ya kuongeza mkataba wa kazi ya ajira ya muda kwa watumishi katika kada za Madereva watatu (3) na Wafanya Usafi wanane (8)
10. Kufunga Kikao

**Muht.Na.66/12/2021- Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 17.11.2021**

Wajumbe waliusoma Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa tarehe 17.11.2021 ukurasa hadi ukurasa na walifanya marekebisho ya makosa ya kiuchapaji kisha waliuthibitisha ili usainiwe kwa ajili ya kumbukumbu ya baadae.

**Muht.Na.67/12/2021- Yatokanayo na Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 17.11.2021**

Wajumbe walijadili utekelezaji wa maazimio ya kikao cha tarehe 17.11.2021 ambapo ufafanuzi ulitolewa kuwa utekelezaji wa maazimio haukufanyika kutokana na mwingiliano wa ratiba na kuwa mkaguzi wa ndani ambaye ndiye alielekezwa kutekeleza maazimio alikuwa kwenye kazi maalum Musoma. Wajumbe walikubaliana kuwa ripoti

ya maazimio hayo iwasilishwe kikao kijacho kitakachojadili taarifa za mwezi Desemba ambapo maazimio yalikuwa kama ifuatavyo:

***MAAZIMIO:***

1. *Iliazimiwa kuwa mkaguzi wa ndani afanye ukaguzi wa matumizi ya fedha za akaunti ya amana kwa kipindi cha uanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2020/2021*

**Muht.Na.68/12/2021 - Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Dharula cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 22.10.2021**

Wajumbe waliusoma Muhtasari wa kikao cha dharula cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa tarehe 22.10.2021 ukurasa hadi ukurasa na walifanya marekebisho ya makosa ya kiuchapaji. Walibaini kuwa muhtasari huo hauna maazimio na kuelekeza kuwa uandikwe upya ukihusisha maazimio ya kikao hicho cha dharula.

**Muht.Na.69/12/2021- Taarifa ya Mapato na Matumizi Mwezi Novemba 2021**

**Kaimu mkuu wa idara ya fedha na biashara kwa niaba ya Mkurugenzi mtendaji(W):** Aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi cha mwezi Novemba 2021 ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema imekisia kukusanya jumla ya Tsh1,800,000,000.00. Halmashauri imefanikiwa kukusanya Tsh 514,256,572.31 kuanzia mwezi Julai 2021 hadi Novemba 2021 sawa na 28.57% ya lengo la mwaka. Mapato ya Halmashauri kwa mwezi Novemba ni kama ifuatavyo:

1. Vyanzo vya ndani vya Halmashauri kwa mchanganuo ufuatao:

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Usafi na Mazingira | Tsh | 847,200.00 |
| ii. | Idara ya Fedha, Biashara na Masoko | Tsh | 60,413,533.60 |
| iii. | Utamaduni | Tsh | 650,000.00 |
| iv. | Idara ya Mifugo na Uvuvi | Tsh | 16,437,700.00 |
| v. | Idara ya Kilimo | Tsh | 2,371,000.00 |
| vi. | Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii | Tsh | 120,000.00 |
| vii. | Idara ya Ardhi na Maliasili | Tsh | 2,781,242.00 |
| | **JUMLA** | **Tsh** | **83,620,675.60** |

2. Vyanzo vya ndani ngazi za chini (mapato fungiwa)..............Tsh 15,853,289.87
3. Mapokezi ya Mishahara..................................................Tsh 2,624,478,150.00
4. Matumizi Mengineyo (OC)..............................................Tsh 1,019,700,000.00
5. Fedha za Miradi ya Maendeleo na Wahisani......................Tsh 3,869,527,077.02

Kiasi cha Tsh 33,448,270.24 kimetengwa kutoka Tsh 83,620,675.60 za vyanzo vya ndani kama 40% ya mchango wa Halmashauri kwenye miradi ya maendeleo.

Kwa upande wa matumizi, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 Halmashauri ilikisia kutumia jumla ya Tsh 1,800,000,000/= katika kutekeleza miradi ya maendeleo, mishahara na matumizi mengineyo. Kwa mwezi Novemba, matumizi yalikuwa kama ifuatavyo:

1. Matumizi mengineyo kupitia vyanzo vya ndani......................Tsh 62,574,000.00
2. Matumizi katika ngazi za chini (mapato fungiwa)..................Tsh 229,929,703.85
3. Matumizi ya mishahara................................................... Tsh 2,624,478,150.00
4. Ruzuku ya matumizi mengineyo (OC)..................................Tsh 38,619,527.00
5. Miradi ya maendeleo na Wahisani ....................................Tsh 381,166,581.00

Vilevile, alibainisha changamoto za mapato ikiwa ni pamoja na tozo ndogo kwa baadhi ya vyanzo ikilinganishwa na majirani wanaoizunguka Halmashauri; minada kukosa uzio; na watoza ushuru wakubwa kutopeleka fedha benki kwa mwezi Novemba baada ya kujua kuwa wanasitishiwa mikataba. Ili kukabiliana na changamoto hizi, menejimenti ilishauri kuwa tozo za samaki ziongezwe kutoka Tsh 100/= hadi 200/= kwa kilo na Tsh 2,000/= kwa gunia la mpunga badala ya Tsh 1,000/=. Menejimenti ilishauri kuwa bajeti itengwe kwa ajili ya kukarabati uzio katika mnada hasa mnada wa Sima. Kisha aliomba kuwasilisha.

Wajumbe waliijadili taarifa ya mapato na matumizi na kushauri kuwa kiasi cha fedha Tsh 33,448,270.24 kilichotengwa kama 40% ya Mchango wa Halmashauri kwenye Miradi ya Maendeleo kupitia vyanzo vya nadani zibaki kwenye akaunti zikisubiri kuongeza wigo wa vifungu. Waliridhia viwango vya tozo vilivyopendekezwa na wataalamu kuwa tozo za samaki ziongezwe kutoka Tsh 100/= hadi 200/= kwa kilo na

Tsh 2,000/= kwa gunia la mpunga badala ya Tsh 1,000/=. Kuhusu watoza ushuru wakubwa kutopeleka fedha benki kwa mwezi Novemba baada ya kujua kuwa wanasitishiwa mikataba, wajumbe walielekeza kuwa mweka hazina aandae taarifa inayobainisha mawakala ambao hawakuwasililisha fedha benki na kamisheni zao ili kuona namna ya kuwalipa. Walielekeza pia iandaliwe ripoti ya mwenendo wa mapato baada ya kuondoa mawakala na kuwatumia watumishi katika ukusanyaji wa mapato. Kuhusiana na kusuasua kwa utekelezaji wa zoezi la kuwalipa wenyeviti wa vijiji kama ilivyoelekezwa kwenye bajeti ya fedha ya jimbo, wataalam walilichukua ili kulifanyia kazi. Walihoji kuhusu Tsh 7,600,000/= fedha za majoho kwa ajili ya waheshimiwa madiwani ambapo utekelezaji wake umechelewa. Walisisitiza kuwa majoho ya waheshimiwa madiwani yanatakiwa yapatikane ili yatumike kwenye Mkutano wa Baraza la Januari 2022. Wajumbe walihoji juu ya mkakati wa Mweka Hazina wa kuinua mapato ya Halmashauri ambapo ufafanuzi ulitolewa kuwa mkakati mmojawapo ni kukusanya mapato duka kwa duka na kufuatilia kwa karibu kila chanzo ndani ya Halmashauri.

**AZIMIO:**

2. *Iliazimiwa kuwa uwasilishwe mpango mkakati wa kukusanya mapato na matokeo yake katika kikao kijacho cha kujadili taarifa za mwezi Desemba.*
3. *Iliazimiwa kuwa mweka hazina aandae taarifa inayobainisha mawakala ambao hawakuwasililisha fedha benki na kamisheni zao ili kuona namna ya kuwalipa.*
4. *Iliazimiwa kuwa iandaliwe ripoti ya mwenendo wa mapato baada ya kuondoa mawakala na kuwatumia watumishi katika ukusanyaji wa mapato.*

**Muht.Na.70/12/2021- Taarifa ya Motor Grader 140K SM11110 ya Halmashauri kwa kipindi cha Mwezi Novemba 2021**

**Afisa Usafirishaji kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji:** Aliwasilisha taarifa ya motor Grader 140K SM11110 la Halmashauri kwa mwezi Novemba 2021 ambapo aliwaeleza wajumbe kwamba grader hilo halijafanya kazi yoyote kwenye kata au ukodishaji kwasababu lilikuwa linafanyiwa matengenezo ya kawaida (minor service) na kuwa tayari limekaguliwa na TEMESA. Aliwafahamisha wajumbe kuwa magurudumu mawili

ya thamani ya Tsh 5,600,000/= yamelipiwa na kupokelewa ila bima ya Tsh 5,428,000/= haijalipwa.

Wajumbe walijadili na kubaini kuwa grader liko nje ya ratiba kwa sababu limekuwa likihitaji matengeneo. Wajumbe walielezwa kuwa changamoto ambazo zimechelewesha mtambo wa Halmashauri kuanza kazi baada ya matengenezo yaliyofanyika ni betri mbili ambazo tayari zimeshaandikiwa na mara zitakapofika mtambo utaanza kufanya kazi. Wajumbe walisisitiza kuwa zipatikane berti hizo ili mtambo uweze kufanya kazi ya barabara katika kata. Walielekeza kuwa mkurugenzi atenge mafuta kwa kazi za dharula ikiwemo kufungua barabara ya kuelekea makaburi ya eneo la Missio. Wajumbe waliipokea taarifa kisha waliridhia.

**Muht.Na.71/12/2021- Taarifa ya mapokezi ya fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha Tsh 886,012,138.30**

**Mkuu wa idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W):** Aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya Tsh 886,012,138.30 kutoka OR-TAMISEMI kupitia mfuko wa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama ifuatavyo:

| NA | IDARA | KIASI CHA FEDHA | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1. | Afya | 416,012,138.30 | • Tsh 300,000,000.00 ujenzi wa jengo la huduma za dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya ya Sengerema<br>• Tshs 90,000,000.00 ujenzi wa nyumba tatu za watumishi katika kituo cha Afya Kagunga<br>• Tsh 6,514,747.00 ufuatiliaji miradi ya afya<br>• Tsh 19,497,391 utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 |
| 2. | Elimu Sekondari | 470,000,000.00 | Ujenzi wa shule ya sekondari kata ya Ibondo ukihusisha:<br>• vyumba 8 vya madarasa<br>• maabara 3 za Sayansi<br>• jengo la utawala |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | • maktaba<br>• chumba cha TEHAMA<br>• vyoo 20<br>• tanki 2 za lita 10,000 za maji<br>• nguzo ya kuweka tanki<br>• miundombinu ya kunawa mikono<br>• miundombinu ya kuvuna au kuunganisha maji<br>• nyumba 2 za walimu<br>• vifaa vya TEHAMA. |

Vilevile alisisitiza kuhusu umakini katika kusimamia miradi hiyo ili thamani ya fedha zilizotolewa ionekane kisha aliomba kuwasilisha.

Wajumbe walipata muda wa kujadili taarifa hiyo na kuhoji sababu za waheshimiwa madiwani kutohusishwa katika suala zima la uhamasishaji wananchi kuchanjwa chanjo ya UVIKO-19. Vilevile walihoji kuhusu mgawo wa fedha za uhamasishaji katika vijiji kwa kuwa haugusi vikundi vyote vya uhamasishaji. Ufafanuzi ulitolewa kuwa kwa mujibu wa mwongozo, fedha za uhamasishaji wa chanjo ya UVIKO-19 hutolewa kwa vikundi vilivyofanya vizuri tu na vyenye matokeo. Hatahivyo, wajumbe walisisitiza kuwa utaratibu katika kuteua vijiji na vikundi vya uhamasishaji uhusishe waheshimiwa madiwani na wenyeviti wa vijiji ili kuleta tija katika utoaji chanjo na kuondoa sintofahamu katika mgawo wa fedha za uhamasishaji.

Wajumbe walionesha kutoridhika na usiri katika suala la wizi wa saruji ambao umetokea mara mbili katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Ufafanuzi ulitolewa kuwa suala hilo liko katika vyombo vya uchunguzi hivyo halipaswi kujadiliwa. Hatahivyo, wajumbe walisisitiza kuwa wao ndio wenye Halmashauri na kuwa wana haki ya kufahamishwa juu ya wizi huo. Hivyo, walimwelekeza mkaguzi wa ndani kuandaa taarifa za wizi wa saruji kwa awamu zote mbili iwasilishwe kwenye kikao kitakachojadili taarifa za mwezi Desemba.

**AZIMIO:**

5. *Iliazimiwa kuwa ufanyike ukaguzi maalum kuhusu wizi wa saruji kwa awamu zote mbili na taarifa iwasilishwe kwenye kikao kitakachojadili taarifa za mwezi Desemba*

**Muht.Na.72/12/2021- Taarifa ya kuongeza mkataba wa kazi ya ajira ya muda kwa watumishi katika kada za Madereva wanne (4) na Wafanya Usafi wanane (8)**

**Mkuu wa idara ya Utumishi na Utawala kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W):** Aliwasilisha ombi la kuongeza mkataba wa kazi ya ajira ya muda kwa madereva wanne na wafanya usafi wanane ambao mkataba wao unaishia tarehe 31.12.2021 kutokana na kuwa bado kuna uhitaji katika kada hizi. Alifafanua kuwa wafanyakazi hawa wameandika barua zisizokuwa na kumbukumbu namba za tarehe 2.12.2021 kuomba kuongezewa mkataba wa kazi sawa na maelekezo ya kifungu cha sita katika kipengele cha masharti mengine ya mkataba wao kinachoeleza kuwa "Endapo mwajiriwa anayo nia ya kuendelea na mkataba mwingine anapaswa kumwarifu mwajiri ndani ya siku thelathini". Malipo ya madereva watatu kati ya wanne kwa mwezi ni Tsh 300,000/=, dereva mmoja kwa mwezi ni Tsh 525,000/= na kila mfanya usafi atalipwa Tsh 150,000/= kwa mwezi. Malipo yote yatafanyika kupitia idara mbalimbali kama ifuatavyo:

| NA | JINA KAMILI | MSHAHARA KWA MWEZI | IDARA ITAKAYOLIPA | ENEO LA KAZI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MUSSA LAURENT | 150,000/= | ELIMU MSINGI | Usafi wa mazingira Idara ya Elimu Msingi |
| 2. | DENIS MUTOKELA | 150,000/= | AFYA | Usafi wa mazingira Idara ya Afya |
| 3. | HELLENA CHARLES | 150,000/= | AFYA | Usafi wa mazingira Idara ya Afya |
| 4. | PETER JOHN | 150,000/= | AFYA | Usafi wa mazingira Idara ya Afya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5. | ANGERINA JOSEPH | 150,000/= | KILIMO/MIFUGO | Usafi wa mazingira Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 6. | ROBERT CHRISTIANE | 150,000/= | UJENZI | Usafi wa mazingira nyumbani kwa Mkurugenzi na Idara ya Ujenzi |
| 7. | SAID RASHID | 150,000/= | MIPANGO, M/JAMII | Usafi wa mazingira Idara ya Maendeleo ya jamii |
| 8. | EDWIN MTWEVE | 150,000/= | ELIMU SEKONDARI | Usafi wa Mazingira idara ya Elimu Sekondari |
| 9. | GABRIEL LUCAS MWENDA | 300,000/= | UTAWALA (mapato ya ndani) | Dereva gari DFPA 0128 la Idara ya Mazingira |
| 10. | MUSSA JULIUS NDEKEJA | 300,000/= | UTAWALA (mapato ya ndani) | Dereva gari SM 3721 la idara ya Elimu |
| 11. | EMMANUEL L. MUNETH | 300,000/= | AFYA | Dereva |
| 12. | MARTINE CHIBA | 525,000/= | AFYA | Dereva gari DFPA1433 la Idara ya Afya |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo kisha waliridhia kuongeza mkataba wa ajira ya muda kwa madereva watatu na wafanya usafi wanane.

**Muht.Na.73/12/2021 – Kufunga Kikao**

**Katibu:** Aliwashukuru wajumbe kwa uvumilivu na kusisitiza juu ya ushirikiano kati ya wataalam na wanasiasa kwasababu wote wanajenga nyumba moja. Pia alisisitiza

kuhusu kuchukuliana na kuvumiliana kwa mapungufu yale ya kibinadamu yanayojitokeza. Alimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kupambania Halmashauri kwa lengo la kuhakikisha inasonga mbele. Alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga kikao.

**Mwenyekiti:** Aliwashukuru wajumbe kwa michango yao. Alimfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa wataalam wamekata tamaa kufanya kazi katika jimbo la Sengerema kutokana na kauli zake. Alimshauri mheshimiwa Mbunge kuwa na mawasiliano ya karibu na wataalam na hasa Mkurugenzi ili anapotoa taarifa zozote awe na uhakika nazo. Alisisitiza kuwa tuhuma dhidi ya wataalam walioko gereza la Butimba si za kweli na kuwa ni makosa ya mhandisi mshauri aliyeshauri vibaya. Aliwaeleza wajumbe kuwa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ndiyo iliridhia matumizi ya fedha katika mradi na kuelekeza utaratibu wote ufuatwe. Alimpongeza Mkurugenzi na timu ya mapato kwa kuhakikisha mapato yanapanda kwa mwezi Novemba. Pia alimpongeza Mkuu wa Kitengo cha Ugavi kwa kujitolea na kuamua kusafiri kwenda Dar es Salaam kufuatilia bati za miradi ya madarasa yanayojengwa katika Halmashauri ya Sengerema. Hata hivyo, aliikosoa idara ya mifugo na uvuvi kwa vyanzo vyao kuwa na mapato ya chini. Hivyo, alishauri kuwa POS zaidi ya sita (6) zipelekwe Jumakisiwani ili kila mwalo uwe na POS. Mwisho aliwatakia heri wajumbe wote katika sherehe za Krismas na Mwakampya kisha alifunga kikao mnamo saa 10:10 jioni.

| | |
|---|---|
| ..................................... | ..................................... |
| Yanga E. Makaga | Binuru M. Shekidele |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**UMETHIBITISHWA LEO TAREHE** 21/01/2022